

# **KILA MTEULE LAZIMA ATENGENEZE MAZINGIRA YA KUBARIKIWA NA BWANA YESU MWAKA 2021.**

## **Mdo 9: 36 – 43, Tito 3: 8**

### **1. UTANGULIZI**

Sifa kubwa ya Mama Dorkasi ni kwamba yeye alijaa matendo mema!! Hakuwa mama wa maneno mengi no!! Ni kama Yesu alivyoundea mtini mzuri wenye majani mengi lakini akakosa matunda na akaulaani siku hiyo hiyo. **Mark 11: 12 – 14.**

- Dorkasi alijaa matendo mema ya upendo kwa kuwajali/kuwasaidia wajane waliokuwa katika uhitaji mkubwa jambo ambalo Mungu alilifurahia sana, na ulipofika wakati wa shida yake Dorkasi (Kufariki) Mungu alisikia kilio cha wajane hawa na akamfufua Dorkasi ili apate kuwahudumia tena. Sijui kama umewahi kujiuliza swali au kujaribu kupata picha ya Dorkasi baada ya kufufuka huduma yake aliiboresha kwa kiwango kipi!!
- Mungu huzuia mauti kwa watenda mema ili vilio vya watendewa visimsumbue hadi anapopatikana mtu mwingine mbadala.

### **2. Mwanamke mwingine ambaye alitengeneza mazingira ya kubarikiwa na Mungu ni huyu - **2Wafal 4: 8 – 17.****

- La muhimu kujua sana ni kwamba unapotenda kwa upendo maadamu una moyo wa kuwajali wahitaji siyo kwamba shetani hataleta matatizo kwako kama ya kuugua au hata kufa Laa hasha; lakini ahadi ya ajabu kwao kutoka kwa Mungu ni kubwa mno. **Zab 41: 1 – 3.**

- Kama tu ilivyokuwa kwa Dorkasi; Mwanamke huyu mshunami naye mtoto wake mpendwa akafa tu ghafla; Ona Elisha nabii alivyotaabika hadi baraka nyingine za huyu mwanamke.

**2Wafalme 4: 18 – 37, 2Wafal 8: 1 - 6**

3. Mwanaume Ayubu alitengeneza mazingira ya Baraka zake za baadaye pale alipowajali sana wajane na yatima na wahitaji wengine. **Ayubu 31: 16 – 21; Ayubu 29: 12.** Mwisho wa Ayubu pamoja na mapito mengi aliyopitia alikuwa mwema ajabu. **Ayubu 42: 10 .** Hata kama kweli Mungu aliruhusu Ayubu ateseke kwa sababu ambazo Ayubu hakuzielewa. Mungu sababu zake kwa Ayubu zilikuwa za Kiroho zaidi, **baraka zake kwa Ayubu mwishowe zilifuta machungu na maumivu yote aliyokuwa ameyapitia Ayubu na akawa na mwisho mwema ajabu;** na kama ni utii na mke wake kumheshimu baada ya taabu hii, naamini utii na heshima vilikuwa vya hali ya juu hata kutoka kwa wale rafiki zake watatu waliomkejeli sana wakati wa mapito yake. Mwisho wetu ndiyo muhimu bila kujali tumepitia yapi. **Mhub 7: 8**

4. Wapo watu wengi katika Biblia ambao walitengeneza mazingira ya baraka zao kama vile Ibrahimu - **Mwanzo 18: 1 – 15, 21: 1 – 7,** Mwanamke Mariamu - **Math 26: 6 – 13 (Yoh 20: 11 – 18,** Mwanamke Abigaili - **1Samwl 25: 23 – 35;** Mtume Barnaba - **Mdo 4: 36 – 37; 9: 26 – 30, 15: 36 – 40.** Tuuone mwaka 2021 kuwa mwaka wa matendo zaidi na maneno yawe machache. **Yak 2: 14 – 26.** Kama matendo mema yanaweza kuachwa swali kwa watendewa tu **(2Wafal 4: 12 – 13,** Mungu je anajiuliza maswali mangapi pale mtu anapojaa matendo mema kwa **wahitaji!!**

- Tumefundishana mno mwaka 2020, mwaka ujao uwe ni wa kujaa matendo mema kama tunataka kuona Mungu wetu akitutendea nasi matendo yatakayowafanya wale wanaotudharau masikio yao yawashe. Amina

**Na**

**Askofu Dr. L. M. Mwizarubi**

**10/01/2021**